**JAMHURIYA MUUNGANO WATANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**MKOA WA LINDI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**

**NICODEMUS BANDUKA SEKONDARI,**
**SLP 80,**
**LIWALE**
**13/12/2020**
**SIMU: 0655808708/0713656481.**

**KUMB.NA.LW/DC/NBSS/JI/2021/004**
**JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………………….............................**
**KIJIJI CHA ..............................................................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YASEKONDARI NICODEMUSBANDUKA ILIYOPO WILAYA YA LIWALE MKOA WA LINDI MWAKA 2021 (JOINING INSTRUCTIONS 2021)**

## 1. UTANGULIZI

Nina furaha ya kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2021Shule ya Sekondari Nicodemus Banduka. Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti hapa shuleni si zaidi ya siku saba (7) tangu shule kufunguliwa. Shule ya hii ipo Kaskazini mwa Mji wa Liwale kilomita ishirini (20 KM) kutoka mjini Liwale barabara iendayo Kikulyungu katika Kata ya Mbaya Tarafa ya Liwale.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### A. SARE YA SHULE

#### i. WAVULANA

- Suruali **mbili ndefu** zakushona rangi ya **udongo (Brown)** upana wa suruali **usipungue inchi 16 (Mfano wa rangi ya kitambaa umeambatanishwa , zingatia rangi na aina yakitambaa)**
- **Tai mbili** ndefu rangi ya suruali
- **Mashati meupe mawili** mikono mifupi
- **Viatu vya ngozi** vyenye visigino vifupi
- Soksi nyeupe pea **TATU** au **zaidi**
- **Mkanda mweusi**
- Sweta rangi**ya bluu/brown**.
- **Kaptula mbili (2)** (bukta) kwa ajili ya michezo,**rangi ya bluu**
- Suruali **mbili nyeus**i kwa ajili ya kazi za nje
- **Tisheti ya shule (inapatikana shuleni sh. 13,000/=)**
- **Fulana mbili nyekundu** isiwe na maandishi na picha yoyote kwa ya ajili ya kazi za nje

#### ii. WASICHANA

- **Sketi mbili** ndefu za kushona **rangi ya udongo (Brown)** ndefu za kufunika miguu yote na zisizobana **(MSHONO UWE RINDA BOKSI)**
  **Mfano wa rangi ya kitambaa umeambatanishwa , zingatia rangi na aina yakitambaa**
- **Mashati mawili** meupe mikono mifupi **(mnaruhusiwa kuvaa hijabu (nyeupe) na nusu kanzu**)
- **Tai mbili** za rangi ya kitabaa cha sketi
- **Sketi mbili nyeusi** kwa ajili ya kazi za nje na michezo
- **Tisheti ya shule (inapatikana shuleni sh. 13,000/=)**
- **Fulana mbili nyekundu** isiwe na maandishi na picha yoyote kwa ya ajili ya kazi za nje na michezo
- **Viatu vyeusi vya ngozi vyenyevisigino vifupi ( viatu aina ya BAJAJI havirusiwi/havitakiwi shuleni)**
- Sweta rangi ya **BLUU**
- **Soksi nyeupe pea nne (4)**

### B. VIFAA VYA MASOMO, KAZI NA MICHANGO MBALIMBALI

Kila **mwanafunzi anapaswa kuja na vifaa vifuatavyo**

- **Madaftari makubwa/Counter (3 QUIRES) books yasiyopungua 10 au zaidi**

- **Kalamu nyeusi/bluu 5,rula 1, mpenseli 5,kifutio 1,Matheamatical set (mkebe) 1**
- **Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili**
- **Jembe1 lenye mpini, panga/ fyekeo na ufyagio**
- **Ream 1 ya karatasi kwa ajili ya mitihani (muhimu sana)**
- **Saa ya mkononi digital au mshale (rangi nyeusi)**

**MUHIMU:**

i. Kwa wale wanafunzi wasio na **BIMA YA AFYA** wazazi mnashauriwa kuchangia Tsh 5000/= kwa ajili ya bima hiyo.

ii. Kwa wanafunzi wanaotoka mbali na shule kama vile Mtawango, Mbuli, Nyera, Kichonda na Liwale Mjini wazazi mnashauriwa kuwapangishia watoto wenu maeneo karibu na shule.

## C. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **sheria ya elimu Na. 25ya mwaka 1978** na kama **ilivyorekebishawa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995**.

Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na **OFISI YA RAIS – TAMISEMI-**yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu na **Wizara ya Elimu, Sayansi,.Tekinolojia na Ufundi -**yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yatakayo fafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.Hivyo kama mwanafunzi unapaswa kuzingatia yafuatayo;

i. **Heshima kwa viongozi, wazazi na wafanya kazi wote wa shule.**
ii. **Mahudhurio na kushiriki vizuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni Lazima.**
iii. **Kuwahi katika kila Shughuli za shule na nyingine utakazopewa.**
iv. **Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.**
v. **Kutunza afya ya mwili,mavazi na mazingira ya shule.**
vi. **Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.**
vii. **Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.**
viii. **Kutunza mali za umma (shule).**
ix. **Mwanafunzi atakae haribu mali ya umma mzazi atawajibika kulipa gharama za mli hizo**

## D. MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha **kufukuzwa shule au kusimamishwa shule kwa muda usiopungua siku ishirini na moja (21)**

a) **Wizi.**
b) **Uasharati.**
c) **Ubakaji.**
d) **Ulevi na atomize mabaya ya dawa za kulevya, kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi n.k.**
e) **Kupigana au kupigana.**
f) **Kuharibu kwa maksudi mali ya umma.**
g) **Kudharau bendera ya Taifa**
h) **Kuwa mjamzito/kupata mimba/kutoa mimba.**
i) **Kuoa au kuolewa.**
j) **Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.**
k) **Kushiriki michezo ya kamari (karata,pool table n.k)**
l) **Kuwa na simu ya mkononi.**

## E. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) **Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni.**
b) **Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.**
c) **Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**…………………..**

**MOHAMED A.S**

**MKUU WA SHULE**

**KIAMBATANISHO NO: 1**

**(A) TAMKO LA MWANAFUNZI KUKUBALI NAFASI NA MKATABA**

**Mimi** ……………………………………………………………………..........................................(jina)

wa……………………………………………….................................................................(Mahali)

nakubali kujiunga kidato cha ………………katika shule ya Sekondari Nicodemus Banduka na nitafuata sheria zote na kanuni za shule na sitashiriki katika migomo ,fujo,utoro, na makosa ya jinai

Ninakubali kuadhibiwa pale nitakapostahili

**SAHIHI**……………………………………………………**TAREHE…**………………………………………….

**(B) TAMKO LA MZAZI / MLEZI KUKUBALI WAJIBU WA KUSOMESHA**

Mimi………………………………………………………………...........(Jina) wa

………………………………………...(Mahali)

ambaye ni mzazi /mlezi wa ………………………………………………………………............(Jina la mwanafunzi). Ninakubali wajibu wa kutekeleza majukumu yanayonihusu mimi mzazi/mlezi wa kumgharamia mwanafunzi mtajwa katika masomo yake. Ninakubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yaliyotolewa na yatakayotolewana shule

**NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI** ……………………………………………

**SAHIHI……………………………………………………TAREHE………/…………/2021**

**KIAMBANATISHO NAMBA 2**

NICODEMUS BANDUKA SECONDARY SCHOOL
P.O BOX 80
LIWALE.

..…/…/2021

TO THE MEDICAL OFFICER
ANY GOVERNMENT HOSPITAL

**Ref…………………………………………………….............(**Name in full**)**

Please may you examine the above named as to his/her physical and mental fitness/unfitness to undertake secondary school studies and other school activities in general.

i. Eyesight
ii. Hearing
iii. T.B Test
iv. Hepatits
v. Pregnancy (for girls)
vi. Any other serious cases

**MEDICAL CERTIFICATION. (To be completed by a government medical officer)**
I have examined the above named and consider that she / he is physically and mentally fit /unfit for full time student.

i. Eyesight…………………………………………….
ii. Hearing……………………………………………
iii. T.B Test…………………………………………………...
iv. Hepatits ....................................................
v. Pregnancy (for girls) ……………………………………….
vi. Any other serious cases……………………………………….
vii.

Yours faithfully,

……………………….

MOHAMED A.S

THE HEAD MASTER

Name of medical officer………………………………………………...........

Signature………………………….

Date……/…../2021

Stamp………………………….